TANGAZO LA SERIKALI Na 111 la tarehe 14/2/2025

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA
(SURA YA 370)

# HATI YA UHAMISHO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

HATI YA UHAMISHO WA UMILIKI WA JENGO LILILOSAJILIWA KWA JINA LA HALMASHAURI YA BIASHARA YA NDANI (BIT) KWENDA BARAZA LA RUFANI ZA KODI (TRAT) NA BODI YA RUFANI ZA KODI (TRAB) YA MWAKA 2025

Sura ya 370 na Sura ya 257

**KWA KUWA**, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa chini ya Umiliki wa Msajili wa Hazina;

Sura ya 370

**KWA KUWA**, Rais anaweza, kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, kumpa Msajili wa Hazina maelekezo ya kuondosha mali za uwekezaji au mali yoyote inayomilikiwa na Msajili wa Hazina chini ya udhamini na Msajili wa Hazina atatekeleza maelekezo hayo;

**NA KWA KUWA**, Serikali imeona kuwa inafaa kwamba Jengo lililopo Mtaa wa Samora, Kiwanja Na. 2167/40 chenye Hati Na. 1860/11 katika Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam kuhamishwa kutoka chini ya umiliki wa Halmashauri ya Biashara ya Ndani (BIT) kwenda kwa Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB);

**HIVYO BASI**, inaelekezwa kama ifuatavyo:

Jina

**1**. Hati hii itaitwa Hati ya Uhamisho wa Umiliki wa Jengo Lililosajiliwa kwa Jina la Halmashauri ya Biashara ya Ndani (BIT) Kwenda Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB), 2025.

Uhamisho wa Jengo

**2**. Jengo lililoainishwa katika Jedwali la Hati hii ambalo kwa sasa linamilikiwa na Halmashauri ya Biashara ya Ndani (BIT), bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, linahamishwa na kumilikiwa na Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB).

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Mkoa | Hati Na. | Hati Miliki na Maelezo ya Kiwanja | Taasisi inayohamishiwa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 1860/11 | Kiwanja Na. 2167/40, Mtaa wa Samora, Wilaya ya Ilala. | Baraza la Rufani za Kodi (TRAT) na Bodi ya Rufani za Kodi (TRAB) |

**KWA AMRI YA RAIS**

Dodoma,
27 Disemba, 2024

MOSES M. KUSILUKA,
*Katibu Mkuu Kiongozi*